# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

## Kikao cha Kwanza – Tarehe 31 Machi, 2026

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

*(Hapa Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Ziliimbwa)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Daniel S. Baran) Alisoma Dua*

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## TAMKO LA AHADI YA UZALENDO KWA WABUNGE WOTE

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge wote walisoma Tamko la Ahadi ya Uzalendo)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**TAARIFA YA SPIKA**

**NAIBU SPIKA:** Taarifa ya Spika kwa mujibu wa Kanuni ya 41(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ya Mwaka 2025.

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu, tarehe 25 Machi, 2026 tulipata msiba mkubwa wa kuondokewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu na Mbunge wa Jimbo la Ismani, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi.  Marehemu William Lukuvi alifia katika Hospitali ya Benjamin Mkapa iliyopo Dodoma alipokuwa akipatiwa matibabu.

Siku ya Ijumaa, tarehe 27 Machi, 2026 mwili wa Marehemu uliagwa katika Viwanja vya Bunge, Dodoma. Shughuli hiyo iliongozwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba na kuhudhuriwa na Spika wa Bunge, Waheshimiwa Wabunge, viongozi mbalimbali wa Serikali, na wananchi wa Dodoma.

Tarehe 28 Machi, 2026 siku ya Jumamosi mwili wa Marehemu uliagwa Jijini Dar es Salaam katika Viwanja vya Karimjee. Shughuli hiyo iliongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Vilevile, siku ya Jumapili, tarehe 29 Machi, 2026 mwili wa Marehemu ulisafirishwa kwenda Iringa ambapo siku ya Jumatatu tarehe 30 Machi, 2026 uliagwa rasmi na viongozi na wananchi wa Mkoa wa Iringa.

Safari ya mpendwa wetu inahitimishwa rasmi leo Jumanne tarehe 31 Machi, 2026 kwa mazishi yanayotarajiwa kufanyika katika Kijiji cha Idodi, Iringa Vijijini. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba anatarajiwa kuongoza mazishi hayo ambapo pia Spika pamoja na Wabunge kadhaa watahudhuria.

Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo desturi yetu na kwa heshima ya Mbunge mwenzetu, Marehemu Mheshimwia William

Vangimembe Lukuvi, ninaomba tusimame kwa dakika moja ili kumkumbuka na kumwomba Mwenyezi Mungu ampokee na ampumzishe kwa amani.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walisimama kwa muda kumkumbuka Marehemu Mhe. William Vangimembe Lukuvi)*

**NAIBU SPIKA:** Bwana alitoa na Bwana ametwaa, jina la Bwana lihimidiwe.

Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na: -

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba nitoe matangazo yaliyopo Mezani.

Kwanza nitaanza na wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; kwanza ni wageni waliokaa Jukwaa la Spika, tunao wageni sita kutoka Bunge la Zambia, Ndugu Loveness Maambo - Kaimu Katibu wa Bunge; Ndugu Dominic Mwinamo – Mkurugenzi, Ofisi ya Katibu wa Bunge; Ndugu Francis Tanganyika - Mkurugenzi Msaidizi, Utawala na Rasilimali Watu; Ndugu Mutinta Mufalali - Mkurugenzi Msaidizi, Masuala ya Afya; Ndugu Maureen Ngala -

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Fedha; na Ndugu Angela Sinkwaya - Afisa Mipango na Uajiri, ahsanteni sana na karibuni sana Bungeni kwetu. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Zuberi Yahaya Mfaume ambao ni wafanyakazi kutoka vijijini Mkoani Morogoro, ahsante na karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 30 wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga ambao ni wahitimu wa darasa la *Political Science* wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wa mwaka 2012, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile ambao ni wafanyabiashara wa madini kutoka Mkoa wa Geita na Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 40 wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe ambao ni Wanamaombi na Wanakwaya kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao wanafunzi 55 wa Kituo cha Muziki kutoka *Dodoma Adventist Polytechnic College,* karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Wabunge wote kuwa utaratibu wa kuomba nafasi ya kuchangia Hoja za Wizara mbalimbali ni kupitia Mfumo wa Bunge Mtandao. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge wote wenye nia ya kuchangia Bajeti ya Waziri Mkuu ambayo itawasilishwa hapa kesho tarehe 1 Aprili, 2026 na bajeti nyingine wanakumbushwa kufanya hivyo sasa kwa kutuma maombi yao kupitia Mfumo wa Bunge Mtandao.

Waheshimiwa Wabunge, wenye changamoto kuhusu ujazaji wa fomu hizo wanaweza kupata msaada kwa Maafisa TEHAMA waliopo ukumbini au *Ground Floor Wing B,* Jengo la Utawala.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo haya, ninaahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 3.16 Asubuhi Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 1 Aprili, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA